

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

Simu: 028 2590162
Fax: 028 2590249
E – MAIL: dedsengerema@ymail.com



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W)
S.L.P 175,
SENGEREMA.

Kumb Na. SDC/CF.40/1/10

Tarehe: 09.04.2020

TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W) imepokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu Hazina **yanye Kumb.Na.CEG.158/327/01/33** ya tarehe **26/03/2020** iliyohusu Taarifa ya Mgao wa Fedha za Utoaji Mkopo Usio na Riba kwa Watumishi wa Halmashauri Fungu 81M4 kwa ajili ya kununua Magari/Pikipiki, Samani na Matengenezo ya Magari/Pikipiki.


Kwa Tangazo hili Watumishi wote mnakaribishwa kutuma maombi kwa ajili ya Mkopo tajwa hapo juu chini ya masharti yafuatayo:-

- i. Mkopaji anatakiwa kubakiwa na 1/3 ya Mshahara wake baada ya Makato ambayo yatarejeshwa kwa kipindi kisichozidi Miezi 72.
- ii. Mkopaji anatakiwa kutuma barua ya maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.
- iii. Barua ya maombi iambatanishwe na Nakala ya Hati ya Mshahara ya sasa(Current Salary Slip).
- iv. **Mikopo hii hainunui deni kutoka Taasisi nyingine za Fedha.**

Aidha viwango vya Mikopo ya Fedha Taslim vimeambatishwa katika Jedwali.

N:B Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **24/04/2020 saa 4:00 asubuhi.**

Limetolewa:


Magesa M. Boniface

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya,
SENGEREMA.

SENGEREMI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
S. L. P. 175
SENGEREMA

Tarehe 09/04/2020